# 11 MPANGO WA KIMAISHA UNAOKUPA USALAMA NA AMANI



Hapana usalama ama amani katika siku zetu hizi.

- Mauaji pamoja na njaa huitishia dunia.
- Mawakala wa kushurutisha matumizi ya sheria bila ya mafanikio hujaribu kudhibiti mauaji mijini na kuzuwia wizi.
- Wanasaikolojia, pamoja na viongozi wa kidini wanatafuta kupata ufumbuzi wa kuongezeka kwa mashaka ambayo imewakamata mamilioni ya watu, lakini wasipate jibu lo lote. Wanapuuzia chimbuko halisi la machafuko na ufumbuzi wa Mtoaji wa maisha aliouonesha.

**1. Je, ni sababu zipi mbili ambazo zimemleta mwanadamu kwenye ukingo wa machafuko?**

*a) Yeremia 2:13. Wamemwacha* ____________________________ .

*b) Isaya 24:5, 5, 6. Wameziasi* ______________________________.

## *MPANGO WA KIMAISHA KWA AJILI YA FURAHA*

**2. Je, ni kanuni gani alizopewa mwanadamu katika Edeni? Mwanzo 2:17, 18, 3.**

*Kanuni za sheria takatifu ya Mungu zilitolewa pale mwanzoni tu. Mwanadamu aliambiwa, "usiibe kutoka katika ule mti," "usitamani." Ndoa pamoja na siku ya mapumziko vilitolewa, pamoja na vinginevyo. Pasipo na sheria, pasingekuwako na dhambi. Warumi 4:15.*

**3. Je, Mungu aliziandika zile Amri Kumi juu ya nini na aliziandika kwa kitu gani? Kutoka 31:18.**

*Aliziandika juu ya* ________________*, kitu kigumu zaidi, kilichoashiria umilele. Ni kitu pekee alichokiandika kwa* ________________ *chake Mwenyewe. Hii inathibitisha* _____________ *wa sheria Yake.*

**4. Zile mbao mbili za sheria ziliwekwa wapi? Kumbukumbu 10:5.**

*Ndani ya* ______________________________________________________________________

*Zile amri ndio msingi wa serikali ya Mungu na mng'ao wa tabia Yake (Zaburi 89:14).*

| MUNGU NI: | SHERIA YAKE NI: |
|---|---|
| Upendo (1 Yohana 4:8) | Upendo (Warumi 13:9, 10) |
| Mtakatifu (Isaya 6:3) | Takatifu (Warumi 7:12) |
| Mwenye haki (Zaburi 129:4) | Ya haki (Kumbukumbu 4:8) |
| Mwema (Zaburi 145:9, 17) | Njema (Warumi 7:12) |
| Wa kweli (Zaburi 89:14) | Ya kweli (Malaki 2:6) |
| Mwaminifu (Kumbukumbu 7:9) | Aminifu (Zaburi 111:7) |
| Wa milele (Zaburi 45:6) | Ya milele (Zaburi 111:7, 8) |

**5. Kusudi halisi la ile sheria ni ipi? Warumi 3:20, 31; 7:7.**

*Ile sheria hutufanya sisi kuitambua* ________________________________________

**6. Je, ni kwa njia ya sheria ipi ambayo tutahukumiwa nayo katika ile hukumu ya mwisho? Yakobo 2:10-12**

______________________________________________________________________

## *MSIMAMO WA YESU KUHUSU ZILE AMRI KUMI ULIKUWAJE?*

**7. Je, ni nani aliyeandika ile sheria pale Mlima Sinai, ni Baba ama ni Mwana? Nehemia 9:12, 13; 1 Wakorintho 10:1-4.** ____________________________________________

**8. Je, unabii ulisemaje juu ya msimamo wa Kristo juu ya sheria?**

*a) Zaburi 40:7, 8. Sheria Yake __________________________ (Yohana 15:10).*

*b) Isaya 42:21. Inasema kuwa Yeye ataitukuza na kuiadhimisha sheria. Tunaposoma Mahubiri ya pale Mlimani, tunaona kuwa unabii huu ukitimilika (Mathayo 5:21, 22, 27, 28, 33-37, 48).*

**9. Je, ni jinsi gani ambavyo alionesha asili ya milele ya ile sheria? Ni nini ambacho kingetokea kwanza? Luka 16:17.**

____________________________________________________________________

**10. Tunathibitishaje katika kumtii Mungu? Yohana 14:15, 21.**

______________________________ *wetu Kwake.*

*Agano jipya hutofautiana na lile la kale katika sheria ile ambayo imeandikwa tu juu ya mawe, lakini ni katika mioyo na akili zetu (Waebrania 10:16).*

*Iwapo mtu anasema ya kwamba anaye mke wake moyoni mwake, hapo anamaanisha nini? Je, ina maana ya kwamba anataka kumtaliki?*

**11. Je, Yesu alimjibu nini yule kijana tajiri pale alipouliza kama afanye nini ili kuurithi uzima wa milele? Mathayo 19:16-19.**

*Ukitaka kuingia katika uzima wa milele,* ________________________________________*.*

**12. Je, ni nani ambao watashangazwa sana katika ile siku ya hukumu? Mathayo 7:21-23.**

*Wale waliosema kuwa* _______________________ *nao wasiyafanye* _________________

**13. Je, yawezekana kuishika sheria ya Mungu?**

*a) Warumi 8:5-8. Wale wayafuatao mambo ya mwili (watu wa kawaida) hawawezi* ______________ ____________________________ *.*

*b) 1 Yohana 5:2-3. Upendo wa Mungu unapojaa moyoni mwetu, tunaona ya kwamba amri Zake hizi wala sio* _____________________*.*

**14. Je, twawezaje kuwatambua wale Wakristo halisi? 1 Yohana 2:3-6.**

____________________________________________________________________

## *HITIMISHO*

Ile sheria ya Mungu ya milele na ikawe ndio mpango wa kimaisha nayo ndio iongoze tabia yetu. Haiwezi kutanguka kama vile alivyo Mungu Mwenyewe.

**15. Je, ni ahadi gani ambayo Mungu awapatia wale wanaozishika amri Zake?**

*a) Kumbukumbu 5:29. Wata*____________________________________*.*

*b) Zaburi 119:165. Mioyo yetu itajawa na amani.*

---

***Uamuzi wangu:*** *Ninakubali ya kwamba zile Amri Kumi ndio tabia ya Mungu na ni msingi wa kiti Chake cha enzi.* ○ *Ndio* ○ *Hapana*

---